# BreastScreen WA

Swahili

**Screening mammography for women with a family history of breast cancer**

## Ukingaji wa Matiti Kupitia Uchunguzi wa Eksrei kwa Wanawake Walio na Historia ya Kansa ya Matiti katika Familia



Shirika la Ukingaji wa Matiti Australia ya Magharibi ni huduma ya bure ya ukingaji wa matiti kupitia uchunguzi wa eksrei kwa wanawake. Ni ukaguzi muhimu wa afya ya wanawake wa umri hamsini hadi sitini na tisa lakini wanawake kwanzia umri wa miaka arobaini wanaweza kuhudhuria. Hiki kijitabu kitaweza kukujibia baadhi ya maswali unayoweza kuwa nayo kuhusu ukingaji wa matiti kupitia uchunguzi wa eksrei ikiwa una ndugu ambaye ameugua kansa ya matiti.

### Ina maanisha nini kuwa na historia ya kansa ya matiti katika familia?

- Mmoja kati ya ndugu zako awe ameugua kansa ya matiti.
- Wakati watu kadhaa wa familia moja wametambulikana kuwa na ugonjwa fulani, ni kawaida kustaajabu kama umerithiwa.
- Kansa ya matiti hairithiwi, lakini jeni hitilafu za kansa ya matiti zinaweza kurithiwa. Mwanamke akiwa na jeni hitilafu huwa hatarini zaidi, lakini hamna uhakika wa kua na kansa ya matiti.
- Kansa ya matiti mara nyingi hutokea kwa bahati tu na haisababishwi na jeni kupitia uzazi. Kansa ya matiti katika familia huhesabia moja hadi tano asili mia ya kansa zote za matiti.

### Thibitisho la hakika kwa wanawake walio na historia ya kansa ya matiti katika familia

Kwa wanawake wengi kugundua ya kwamba wana historia ya kansa ya matiti katika familia huwa ni jambo la kuhangaisha. Kwa hali yoyote ni muhimu kukumbuka kwamba:

- 1 kati ya wanawake 9 wa Australia watapata kansa ya matiti maishani mwao.
- Kansa ya matiti ni ugonjwa wa kawaida unaohusishwa sana na umri. Kwa idadi ya wanawake wengi hii hutokea kwa bahati tu sio kwa sababu ya historia katika familia.
- Kuwa na mama au ndugu wa kike aliye na kansa ya matiti haimaanishi kwamba wewe pia lazima utaipata kansa ya matiti bila shaka.
- Kuwa na kansa ya matiti haimaanishi ulirithi jeni hitilafu bila shaka, au utaieneza kwa watoto wako.
- Wanawake wanaokaribia tisa kwa kila wanawake kumi wanaopata kansa ya matiti hawana historia ya kansa ya matiti katika familia.

### Historia katika familia yako huwa ya muhimu zaidi wakati:

- zaidi ya ndugu mmoja kwa upande mmoja wa familia (upande wa mama au baba) ametambulikana kuwa na kansa ya matiti.
- hao ndugu walikuwa na umri usiozidi miaka hamsini walipotambulikana mara ya kwanza kuwa na ugonjwa huo.
- hao ndugu walio na kansa ya matiti wana uhusiano wa karibu sana nawe (ndugu wa kike heri kushinda binamu).
- kuna kansa ya matiti yote mawili, kansa ya matiti ya wanaume, au kansa ya matiti na ya ovari katika familia.

**For an appointment phone 13 20 50**

## Je kuwa na historia katika familia kunanisingiziaje kwa kupata huduma kutoka kwa Shirika la Ukingaji wa Matiti hapa Australia ya Magharibi (BreastScreen WA)?

Shirika la Ukingaji wa Matiti Australia ya Magharibi hushauria vipimo vya matiti kupitia eksrei kila baada ya miaka miwili hasaa kwa wanawake wa umri wa miaka hamsini hadi sitini na tisa, kama vile utafiti unadhihirisha ya kwamba vipimo hivyo vina faida kuu zaidi kwa kundi la wanawake wa huo umri. Wanawake wa miaka arobaini hadi arobaini na tisa na wale walio zaidi ya miaka sabini wanakaribishwa pia kuhudhuria ili wafanyiwe eksrei za matiti.

Shirika la Ukingaji wa Matiti Australia ya Magharibi hukusanya habari kuhusu historia katika familia wakati wa vipimo. Kwa idadi chache ya wanawake, namna ya historia katika familia huenda ikaamrisha wao kuhudhuria mara kadhaa ili wapate kupimwa.

## Je kama nina historia katika familia ya kuwa na kansa ya matiti, ni kwa umri gani ninapashwa kuanza vipimo, na mara ngapi ninapashwa kupimwa?

Wanawake kwanzia miaka arobaini ambao wana historia kuu katika familia ya kansa ya matiti wanafaa kupimwa kila mwaka kama wana moja kati ya yafuatayo:

- Ndugu wa karibu sana (mama, ndugu wa kike, binti, baba, mtoto wa kiume, ndugu wa kiume) aliyetambuliwa kuwa na kansa ya matiti kabla ya kutimiza miaka hamsini.
- Ndugu wa karibu sana aliye na kansa kwa matiti yote mawili (iliyotambuliwa kwa umri wowote).
- Ndugu wawili au zaidi wa karibu sana walio na kansa ya matiti (iliyotambuliwa kwa umri wowote).

Wanawake walio na ndugu wa karibu sana ambaye ana kansa ya matiti na ana miaka zaidi ya hamsini, HAWAKO kwa hatari zaidi kushinda mwanamke mwingine yeyote wa kawaida katika jamii. Wanawake hawa wanaalikwa kufanyiwa kipimo cha eksrei ya matiti kila baada ya miaka miwili.

## Je nifanye nini zaidi?

Ukiwa una hangaiko kuhusu historia katika familia ya kansa ya matiti, unapashwa kuzungumzia daktari wako wa familia kuhusu hali ya mambo yako binafsi. Kama kuna tokeo lipya limetambulikana la kansa ya matiti katika familia ni muhimu ujulishe Shirika la Ukingaji wa Matiti Australia ya Magharibi na pia daktari wako wa familia.

## Kumbuka, Ufahamu Kuhusu Matiti:

- Tazama na kugusa matiti ili kutambua mabadiliko yo yote yasiyo ya kawaida kwako.
- Muone daktari wako wa familia mara tu ukiona mabadiliko yoyote ya matiti.
- Muulize daktari wako wa familia kukagua matiti yako kila mwaka.

## Maswali yoyote?

Watumishi wa Shirika la Ukingaji wa Matiti Australia ya Magharibi wako tayari kukujibia maswali yoyote uliyonayo. Tafadhali piga simu nambari (08) 9323 6700 au kwa wanawake wa bara piga simu isiyo ya malipo nambari 1800 800 033. TTY namba ni 1800 241 708.

**Unaweza kufanya agizo kwa kupiga 13 20 50 (kwa malipo ya simu ya mtaa)**

Ukihitaji mfasiria wa bure, tafadhali kwanza pigia Shirika la Huduma ya Tafsiri na Ufasiri (TIS) kwa namba 13 14 50 na kuomba uunganishwe na huduma yetu kwa namba 13 20 50.


GOVERNMENT OF WESTERN AUSTRALIA Department of Health

BreastScreen WA — WA's only accredited screening service

BreastScreen AUSTRALIA — A joint Australian, State and Territory Government Program

**www.breastscreen.health.wa.gov.au**



© BreastScreen WA, Department of Health



Telephone (08) 9323 6700 Facsimile (08) 9323 6799 TTY 1800 241 708 Bookings 13 20 50



OA004196 OCT'11